

VodaFibre – nyongeza ya sera ya faragha

Hii nyongeza ya sera ya faragha inatoa taarifa za jumla katika shughuli iliyofanyika kwa bidhaa ya VodaFibre, kujenga mazingira zaidi katika [sera kuu ya faragha](#). Iwapo unatumia VodaFibre na Simu pamoja na huduma nyingine, unapaswa kusoma taarifa za faragha za huduma nyingine vilevile.

Iwapo utakuwa na maswali yoyote katika vipengele vya nyongeza hii ya faragha, tafadhali piga simu 100 au tembelea maduka yetu ya Vodacom au madawati ya Huduma kwa Wateja na mmojawapo katika timu yetu maalum atakujibu.

VodaFibre

VodaFibre hutoa huduma ya muunganisho wa intaneti kupitia miundombinu ya nyaya za fibre-optic. Utahitajika kutoa idhini kwa kununua kifurushi cha huduma na kuruhusu ufikiaji wa nyumba yako kwa ajili ya usakinishaji.

Taarifa binafsi tunazochukua kukuhusu wewe

- Namba yako ya simu ya mkononi
- Taarifa za akaunti yako, kama vile aina ya usajili, njia ya malipo (M-Pesa), aina ya mteja, tarehe za malipo na tarehe ya kuisha kwa kifurushi
- Anwani yako ya barua pepe
- Taarifa zako za mahala ulipo,
- Taarifa za huduma kwa wateja zinazotokana na mawasiliano yako nasi
- Taarifa kuhusu matumizi yako ya huduma, kama vile matumizi ya data
- Taarifa zako zinazohusiana na kifurushi unachotaka kufuatilia.

Pia tunakusanya taarifa kuhusu jinsi unavyotumia bidhaa na huduma zetu, ikiwa ni pamoja na:

- Kiwango cha huduma unachopokea, kwa mfano matatizo ya mtandao au huduma na matukio mengine yanayoweza kuathiri huduma zetu za mtandao
- Tunakusanya pia taarifa za uchambuzi zisizo na utambulisho kuhusu jinsi watumiaji wanavyotumia bidhaa ya VodaFibre, kwa lengo la kuboresha uzoefu wako na kusaidia kutambua na kutatua changamoto za kiufundi

Wakati gani tunachukua taarifa zako binafsi

- Unapojisajili na kujiunga na huduma
- Unapotumia Programu au tovuti na hatua zake mbalimbali, kama vile kupakua maudhui
- Unapowasiliana na timu yetu ya huduma kwa wateja kwa maswali au msaada
- Unapolipia huduma

Vodacom itatumia taarifa zako binafsi kwa kuzingatia:

Kuhakikisha Huduma ya Kifurushi Chako na Mahitaji Yako Yanatekelezwa. Kwa mfano, tunahitaji kuchakata taarifa za matumizi ya mtandao wako ili kifaa chako kiweze

kuunganishwa, na tutahitaji pia kuchakata taarifa za malipo za Msimamizi kwa ajili ya kutoza ada ya kila mwezi.

Maslahi halali ya kibiashara ya Vodacom, kwa mfano, kuzuia udanganyifu, kuimarisha usalama wa mtandao na huduma, matangazo ya moja kwa moja, na uboreshaji wa huduma zetu. Kila tunapozingatia msingi huu halali kuchakata data zako, tunatathmini maslahi yetu ya biashara kuhakikisha kuwa hayazidi haki zako. Pia, kuna wakati unakuwa na haki ya kukataa hii michakato. Kwa taarifa zaidi, tembelea kipengele cha Haki Zako katika sera hii.

Utekelezaji wa matakwa ya lazima ya kisheria, ikiwa ni pamoja na matakwa ya kihalisi na kodi, ambayo yako chini ya sera madhubuti za ndani (kama vile muda wa kutunza taarifa), taratibu, na haki yako ya kuweka mipaka ya matumizi ya data, ambayo inadhibiti wigo wa msaada wa kisheria utakaotakiwa kutolewa; au

Ridhaa unayotoa pale ambapo Vodacom haijiegemezi kwenye msingi wowote wa kisheria. Ridhaa hiyo inaweza kuondolewa muda wowote.

Namna tunavyotumia taarifa zako binafsi

Tunatumia taarifa zako kwa ajili ya kutoa huduma na kutimiza manunuzi yoyote uliyofanya, ikiwa ni pamoja na:

- Kukutambua wewe na akaunti zozote ulizonazo nasi
- Kukuwezesha kupata na kutumia huduma
- Kutoza bili na kutoa huduma kwa wateja
- Kukujulisha kuhusu mabadiliko yoyote kwenye Programu au tovuti au kwenye huduma zetu yanayoweza kukuathiri
- Kuthibitisha utambulisho wako

Kutangaza na Kuunda makundi kulingana na sifa (Profiling)

Ikiwa umeamua kujiunga kupokea matangazo na umetupa ruhusa ya kutumia data yako kutengeneza kipekee ujumbe kuhusu taarifa hizi, tutatumia mwingiliano wako na Programu hii au programu ingine kukujulisha aina ya matangazo tutakayo kutumia ambayo ni muhimu zaidi kwako. Chagua kujiondoa kwenye ujumbe wa matangazo au makundi kulingana na sifa.

Ikiwa hautaki tena kupokea ujumbe wa matangazo kutoka Vodacom, unaweza kuchagua kujiondoa kupokea ujumbe wa matangazo yote au kwa njia uliochagua tu (barua pepe, ujumbe wa mfupi wa maandishi, simu au chapisho).

Kuna njia mbali mbali za kujiondoa:

- Wasiliana na timu yetu ya huduma kwa wateja kwa kupiga 100;

- Ujumbe wetu wote wa matangazo huja na sehemu ya “kujiondoa” ambapo unaweza kubofya ili kujiondoa;
- Mwambie mshauri hutaki matangazo tena, ikiwa utapokea simu ya matangazo;
- Tuma barua pepe kwa customercare@vodacom.co.tz kwa mwongozo
- Kujiondoa hakumaanishi kwamba hautapokea tena ujumbe unaohusiana na huduma, kama vile ujumbe unaokuambia juu ya huduma ulioitaka au vigezo na masharti yetu yanapobadilika. Bado utaendelea kupokea hizo (isipokuwa kama utaonyesha vinginevyo). Unaweza pia kupokea matangazo kupitia taarifa za kushinikiza ikiwa haujazuia kupitia mipangilio yako ya Programu.

Kuboresha huduma zetu

Tunachukua taarifa zisizo bainisha majina au taarifa binafsi za jumla ili kuboresha huduma tunazotoa kwa kila mmoja. Hakuna taarifa zozote za uchambuzi zinazorudi kwako kwa njia yoyote ile.

Kulinda mitandao yetu na kusimamia idadi za simu, ujumbe na matumizi mengine ya mitandao yetu. Kwa mfano, tunabainisha muda ambao mawasiliano hufanywa kwa wingi ili tuweze kujaribu na kuhakikisha kwamba mitandao inakuwa na uwezo wa kuhimili idadi katika muda huo;

Kufahamu namna unavyotumia mitandao, bidhaa na huduma zetu. Kwa kufahamu hivyo, tunaweza kupitia upya, kuendeleza na kuboresha mitandao, bidhaa na huduma hizo, kuanzisha bidhaa na huduma nzuri zaidi, pamoja na kukupa bidhaa na huduma zetu maalum kwako.

Namna tunavyoshirikisha wengine taarifa zako binafsi

Pale inapohusika, tunashirikiana taarifa kuhusu wewe na:

- Kampuni zilizo katika Vodacom Group
- Washirika au mawakala wanaohusika kukupatia bidhaa na huduma ulizomba au ulizotumia;
- Makampuni yanayohusika kutoa huduma kwa ajili ya, au kwa niaba ya, Vodacom Tanzania Public Limited Company, Vodacom Group or Vodafone Group;
- Kumbukumbu za mikopo, mawakala/taasisi za kuzuia udanganyifu au taasisi za kutathmini biashara, au taasisi za kutathmini mikopo;
- Mawakala wa kukusanya madeni au taasisi zingine za kukusanya madeni;
- Taasisi za kusimamia sheria, taasisi za serikali, mamlaka za udhibiti, mahakama au mamlaka zingine za umma endapo tutalazimika, au kuruhusiwa na sheria;
- Upande wa tatu au taasisi ambayo taarifa hizo zinahitajika ili kutekeleza sheria yoyote husika, au matakwa yoyote ya kisheria au ya udhibiti;
- Upande wa tatu kwa ajili ya kufanya matangazo kwa ushirikiano na upande huo;

Kuhamisha taarifa zako binafsi nje ya nchi

Hatuhamishi taarifa zako binafsi kwenda nje ya Tanzania; taarifa binafsi zote zimehifadhiwa kwenye mifumo inayosimamiwa na Vodacom.

Kuweka salama taarifa zako binafsi

Tuna timu maalum za wataalam wa usalama ambazo kila wakati zinapitia na kuboresha njia za kulinda taarifa zako binafsi dhidi ya kupatikana bila idhini, kupotea kwa bahati mbaya, kuvuja au kuharibika.

Mawasiliano kwa njia ya mtandao (kama barua pepe) hayako salama ikiwa hayakuwekewa ulinzi. Mawasiliano yako yanaweza kupita nchi nyingi kabla ya kufika ulikoyatuma, kwani ndiyo mtandao ulivyo.

Hatutakubali kuwajibika endapo taarifa binafsi zitapatikana au kupota bila idhini nje ya uwezo wetu wa kudhibiti.

Kamwe hatutakutaka utupe kwa njia zisizo sahihi taarifa zako binafsi au za akaunti ulizoziwekea ulinzi. Unawajibika kutunza taarifa zako binafsi na za akaunti yako na kutozishirikisha kwa watu wengine.

Tovuti yetu inaweza kutoa mawasiliano ya kimtandao kwa tovuti zingine. Hatuwezi kuwajibika kwa usalama na maudhui ya tovuti za upande wa tatu. Kwa hiyo hakikisha unasoma sera ya kampuni juu ya faragha na vidakuzi kabla ya kutumia au kuweka taarifa zako binafsi kwenye tovuti zao.

Masharti haya yanahusika pia kwa tovuti za upande wa tatu au maudhui unayojiunganisha nayo ili kutumia bidhaa na huduma zetu.

Unaweza kuchagua kutoa taarifa zako kwa njia zingine kama viunganishi vya kijamii (social plug-ins) zikiwemo zile zinazotolewa na Google, Facebook, Twitter na Pinterest) au kwa kutumia huduma za upande wa tatu ambazo zinakuruhusu kutuma maoni au taarifa nyingine za wazi, na upande wa tatu unaweza kutumia taarifa hizo.

Ukomo wa muda wa kutunza taarifa zako binafsi

Tutatunza taarifa zako kwa muda wote ambao sheria itatutaka. Endapo hakuna matakwa ya kisheria, tutazitunza kwa muda ambao tunahitaji tu. Kwa taarifa zaidi ya muda tunaotunza taarifa zako angalia [hapa](#).

Haki zako

Haki ya Kurekebisha taarifa zako binafsi

Una haki ya taarifa zinazokuhusu kusahihishiwa endapo hazina usahihi. Endapo taarifa zako tulizonazo zitahitaji kubadilishwa, au unadhani si sahihi, unaweza kutembelea maduka yetu au madawati la huduma kwa wateja ili kubadilisha.

Haki ya kupata taarifa binafsi

Haki ya kuomba kupata nakala ya taarifa zako ambazo Vodacom inazo. Kuomba taarifa hizi kama mtu binafsi au upande wa tatu ulioidhinishwa, tafadhali tembelea maduka yetu ya Vodacom au madawati ya Huduma kwa Wateja.

Haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kukuathiri

Una haki ya kuitaka Vodacom kusitisha au kutoanza uchakataji wa taarifa yako binafsi yoyote inayokuhusu ikiwa uchakataji huo unaweza kusababisha madhara makubwa kwako au kwa mtu mwingine.

Haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya biashara

Una haki, katika hali fulani, kupinga au kumzuia Vodacom kuchakata taarifa zako za kibinafsi kwa madhumuni ya matangazo ya biashara. Ikiwa hutaki tena kupokea ujumbe wa matangazo ya biashara kutoka kwa Vodacom, unaweza kuchagua kujiondoa kwenye mawasiliano yote ya matangazo ya biashara kwa kujiondoa kupitia CPM kwenye Programu ya Myvodacom na tovuti ya Vodacom, barua pepe, SMS, MMS, kupiga simu kwa kituo cha huduma kwa wateja au chapisho).

Kwa habari zaidi au kutumia haki hii, tafadhali piga simu namba 100 au tembelea maduka yetu ya Vodacom au madawati ya Huduma kwa Wateja.

Haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa Kiotomatiki

Una haki ya kumtaka Vodacom kuhakikisha kwamba uamuzi wowote unaofanywa na Vodacom au kwa niaba ya Vodacom ambao una athari kubwa kwako, haitegemei uchakataji kwa njia ya kiotomatiki pekee.

Haki ya kufutiwa, kuzuia au kuharibu taarifa

Katika mazingira fulani, kwa mfano, tukiwa hatuna tena sababu ya msingi ya kuendelea kushughulika na taarifa zako au hatuhitajiki na sharia kutunza taarifa hizo, unaweza kuomba tuzifute, tuzizuie au kuziharibu.

Haki ya Fidia

Una haki ya kulipwa fidia na Vodacom endapo utapata madhara kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti ya sharia ya Ulinzi wa taarifa wa binafsi uliofanywa na Vodacom.

Namna ya kuwasilisha malalamiko

Endapo una malalamiko, unaweza kuwasiliana nasi kwa kupiga simu 100 au barua pepe customercare@vodacom.co.tz. Pia unaweza kutembelea maduka ya Vodacom au

madawati ya Huduma kwa Wateja. Tutafanya tuwezavyo ili kukusaidia lakini ikiwa bado huna furaha, unaweza kuwasiliana na Tume ya Kulinda Data ya Kibinafsi.

Kwa Masuala ya Faragha/Malalamiko: Tuma barua pepe kwa dataprotectionqueries@vodacom.co.tz au tuma malalamiko kwa anwani yetu ya posta

Vodacom Tower, Ghorofa ya 7, Ursino Estate,

Barabara ya Bagamoyo, S.L.P 2369,

Dar es Salaam.